



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini – Tarehe 14 Juni, 2021

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

- I. **TAARIFA YA SPIKA:**
- II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022.

- III. **MASWALI:**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

79. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais,
Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za
SMZ:

Serikali ilianzisha mpango maalum wa ugatuzi kwa lengo la kurahisisha huduma za kiutendaji kupitia Halmashauri zake za Wilaya.

- (a) Je, Serikali imeshafanya tathmini kujionea mafanikio au changamoto zilizopo juu ya uwepo wa mpango huo.
- (b) Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kuhakikisha inatatua changamoto zilizojitokeza tokea kuanzishwa kwa ugatuzi.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

24. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Soka la Wanawake kwa sasa ni jambo la kimataifa na lenye nafasi kubwa katika medani ya kimichezo. Kwa kulifahamu hilo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TFF tayari wameanzisha ligi mbali mbali za wanawake na baadhi ya timu zimesajili wachezaji wa kulipwa kutoka nchi mbali mbali.

Je, ni sababu gani za msingi zinazoifanya ZFF hadi leo hii ishindwe kuwahamasisha wanawake wa Zanzibar kuanzisha timu za mpira wa miguu na hatimaye kuanzisha ligi mbali mbali hapa Zanzibar.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

183. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Shirika la Biashara la Taifa lilitarajia kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa kiwanda cha kusarifu mwani.

Je, lengo hilo limefikia hatua gani mpaka sasa.

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

165. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii,
Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi, Serikali imejiimarisha katika kujenga hospitali na vituo vya afya ili kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Pamoja na kujengwa kwa hospitali na vituo hivyo, changamoto ya uwepo wa madaktari na vifaa tiba imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza madaktari katika vituo vya Afya vya JKU Wawi na Mvumoni Furaha.
- (b) Je, Serikali haioni haja ya kuirasimisha Bima ya Afya kutumika kwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- (c) Je, Serikali imejipanga vipi kuondoa changamoto ya upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali za Pemba hasa ikizingatiwa kuwa vifaa hivyo ni muhimu katika kutatua changamoto zinazotokana na magonjwa mbali mbali.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

92. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya
Amali:

Je, kuna mpango gani wa kuongeza mishahara kwa walimu baada ya kurudi masomoni.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

104. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika ujenzi wa barabara ya Makoba Kiongwe wananchi wa shehia ya Kidanzini, Makoba na Mafufuni walikatiwa vipando vyao na hadi sasa bado hawajalipwa.

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha wanazodai wananchi hawa.
- (b) Kwa kuwa muda umeshakuwa mrefu, Je, unawaambia nini wananchi wa maeneo hayo.
- (c) Ni lini watalipwa fedha zao.

144. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali inaendelea kufanya juhudi mbali mbali za kuendelea kuzijenga barabara zake Unguja na Pemba kupitia kampuni mbali mbali za ujenzi.

- (a) Je, ni vigezo vipi vinavyochukuliwa na Serikali kuwapatia wakandarasi hao wa ujenzi wa barabara hizo.
- (b) Je, Wizara haioni kuwa vigezo hivyo vinastahiki kuboreshwa zaidi ili kuendana na wakati.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022 na Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya
Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
14 Juni, 2021.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.